

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA RAIS - TAMISEMI**



**TAARIFA KWA UMMA KUHUSU AJIRA YA WALIMU WA  
SHULE ZA MSINGI NA SEKONDARI APRILI, 2019**

**Ndugu Wanahabari**, Ofisi ya Rais - TAMISEMI ilipata kibali cha kuajiri jumla ya walimu **elfu nne mia tano arobaini na tisa (4,549)**. Kibali hicho kilikuwa ni kwa ajili ya walimu wa Shule za Msingi na Sekondari.

**Ndugu Wanahabari**, jumla ya waombaji **91,108** walijitokeza kutuma maombi ya nafasi mbalimbali zilizotangazwa. Kati ya hao, maombi **43,770** sawa na asilimia **48.04** ya waombaji wote yalikuwa na viambatisho vyote vilivyohitajika na jumla ya waombaji **47,338** sawa na asilimia **51.96** maombi yao hayakuwa na vigezo ikiwa ni pamoja na kukosa viambatisho muhimu vilivyohitajika.

**Ndugu Wanahabari**, kutokana na mahitaji makubwa ya walimu katika Shule za Msingi na walimu wa Shule za Sekondari wa masomo Sayansi (Fizikia, Kemia na Baiolojia) na Hisabati, Ofisi ya Rais-TAMISEMI imefanya uchambuzi na kutoa kipaumbele katika ajira ya walimu wa kada zifuatazo:

- (i) Walimu Daraja la Tatu A (Cheti) kwa ajili ya kufundisha Shule za Msingi;
- (ii) Walimu Daraja la Tatu B (Stashahada) wa masomo ya Sayansi kwa ajili ya kufundisha Shule za Sekondari Kidato cha Kwanza hadi cha Nne;
- (iii) Walimu Daraja la Tatu C (Shahada) wa masomo ya Sayansi kwa ajili ya kufundisha katika Shule za Sekondari Kidato cha Tano na Sita; na,
- (iv) Walimu Daraja la Tatu C (Shahada) wa masomo ya Elimu Maalumu, Biashara, Uchumi, Kilimo na Maarifa ya Nyumbani (*Home Economics*) kwa ajili ya kufundisha Shule za Sekondari.

**Ndugu Wanahabari**, mchakato wa kupitia maombi ulijumuisha uhakiki wa uhalali wa vyeti vya Elimu na Taaluma vya waombaji na ukamilifu wa nyaraka zilizohitajika.

**Ndugu Wanahabari**, napenda kutumia nafasi hii kuwataarifu waombaji wote wa masomo ya Sanaa, Sayansi na masomo mengine ambao walitimiza vigezo na hawakufanikiwa kupata nafasi katika kipindi hiki kuwa, maombi yao yote yamechambuliwa na yamehifadhiwa kwenye kanzidata yetu na kuwa, fursa za ajira zitakapojitokeza utaratibu wa ajira utatolewa.

Napenda kuutarifu umma kuwa, jumla ya walimu **4,549** wamepangiwa moja kwa moja kufundisha katika Shule mbalimbali za Msingi na Sekondari nchini zilizokuwa na upungufu mkubwa wa walimu. Kati ya walimu hao, jumla ya walimu **3,059** sawa na asilimia **67.25** wamepangwa kufundisha Shule za Msingi na walimu **1,490** sawa na asilimia **32.75** wamepangwa kufundisha Shule za Sekondari.

**Ndugu Wanahabari**, Walimu wote waliopata ajira wanatakiwa kuripoti kwa Wakurugenzi wa Halmashauri zilipo shule walizopangwa kwa ajili ya uhakiki wa vyeti halisi vya elimu na taaluma, kujaza mikataba ya ajira na taratibu nyingine za kiutumishi na kisha kuripoti katika shule walizopangiwa.

**Ndugu Wanahabari**, napenda kuwataarifu kuwa, walimu wote waliopata ajira wanatakiwa kuripoti katika vituo vyao vya kazi kuanzia tarehe **07 Mei, 2019** hadi **21 Mei, 2019**. **Walimu wapya ambao hawataripoti katika vituo vyao vya kazi ifikapo tarehe 21 Mei, 2019** nafasi zao zitajazwa mara moja bila kuwataarifu kwa kuwapanga walimu wenye sifa ambao hawakupangwa katika awamu hii. Aidha, Wakurugenzi wa Halmashauri wasibadilishe vituo vya kazi vya walimu hao bila KIBALI MAALUM cha Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais - TAMISEMI. Mwajiriwa atakayeripoti na kuchukua posho ya kujikimu kisha akaondoka katika kituo chake cha kazi alichopangiwa atachukuliwa hatua kali za kisheria.

**Ndugu Wanahabari**, mwisho, niwaombe Wakurugenzi wote wa Halmashauri zilizopangiwa walimu wa ajira mpya kuwapokea walimu hao na kukamilisha taratibu za ajira kwa kuzingatia Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo inayosimamia Utumishi wa Umma.

Ahsanteni kwa kunisikiliza.

Selemani Said Jaffo (Mb)  
**WAZIRI WA NCHI**  
**OFISI YA RAIS - TAMISEMI**  
**27 Aprili, 2019**